# MUHTASARI WA MKUTANO WA MASHAURIANO NA WADAU WA NDANI ULIOFANYIKA TANZANIA KATI YA TAREHE 23 APRILI 2025 NA 25 APRILI 2025.

## UTANGULIZI

Effective Climate Solutions 1 FZCO ("ECCS1") na washirika wake wanawaalika wadau kupitia matokeo ya Mashauriano ya Wadau wa Ndani yaliyofanyika kuanzia tarehe 23 Aprili hadi 25 Aprili 2025 katika maeneo ya Ilala, Ubungo na Temeke - Tanzania.

Katika mikutano hiyo ya wadau, Effective Climate Solutions 1 FZCO ("ECCS1") na washirika wake walitambulisha shughuli zao za Mradi wa Hiari wa Kupunguza Kaboni zinazohusu usambazaji wa majiko bora yenye ufanisi wa hali ya juu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Shughuli hizi za Mradi wa Hiari (VPAs) zimejumuishwa chini ya Mpango wa Shughuli wa Viwango vya Dhahabu (Gold Standard Programme of Activities - PoA) uitwao "Mpango wa Ufumbuzi wa Kupika kwa Umeme wa dMRV wa Afrika.

## KUMBUKUMBU ZA MKUTANO

### Usajili:

Washiriki waliwasili na waliombwa kusaini orodha ya mahudhurio. Washiriki waliounganishwa kupitia kiungo cha Zoom walijiandikisha mtandaoni ili kufikia mkutano.

### Hotuba ya Karibu:

Washiriki waliokuwepo kwa njia ya ana kwa ana walikaribishwa na viongozi wa timu ya ECC katika mikutano yote. Utambulisho wa washiriki waliokuwepo kimwili na wale waliojiunga kwa njia ya mtandao ulifanyika. Madhumuni ya mkutano pamoja na ajenda vilielezewa kwa hadhira.

### Uwasilishaji wa Mradi:

Effective Climate Solutions 1 FZCO ("ECCS1") na washirika wake walianza wasilisho lao kwa kuelezea mradi kwa kina; waliwasilisha malengo makuu ya mpango huo na manufaa yake kwa jamii za wenyeji, pamoja na teknolojia ya majiko bora (ICS) inayotumika katika mradi huu.
Pia walitumia muda kuwahamasisha wadau kuhusu mabadiliko ya tabianchi na sababu zake, na walielezea kwa kifupi dhana ya mikopo ya kaboni, masoko ya kaboni na maendeleo ya miradi ya kaboni.
ECCS1 pamoja na washirika wao walioteuliwa walichukua muda kuwaeleza kwa makini wadau kwamba haki za mikopo ya kaboni inayozalishwa kwa kutumia majiko hayo zitahamishiwa kwa ECCS1 kama Shirika linaloratibu na kusimamia mradi mzima. Ufafanuzi wa kuachia haki za mikopo ya kaboni ulionyeshwa kupitia utepe uliowekwa kuzunguka sanduku la jiko, na kipande cha karatasi kilichowekwa kwenye sehemu ya kufungulia sanduku la jiko. Kwa kukata utepe/kipande hicho au kwa kusaini fomu za ridhaa ya kaboni, mtumiaji wa mwisho anakuwa ameachilia madai yake yoyote juu ya punguzo la uzalishaji wa kaboni lililothibitishwa linalozalishwa kwa kutumia jiko hilo. Lengo la mpango huu na jinsi ambavyo ECCS1 itatumia mapato yatokanayo na mauzo ya mikopo ya kaboni vilielezwa kwa uwazi katika uwasilishaji wakati wa mkutano wa Mashauriano ya Wadau wa Ndani (LSC).

**Maswali na Majibu:**

Wadau walitoa maswali mengi kuhusu bei ya majiko bora (ICS) na ubora wake, pamoja na muda unaotarajiwa wa utekelezaji wa mradi na mipango ya usambazaji. Walionesha nia kubwa katika ushirikishwaji wa jamii, hasa ushiriki wa wanawake.

Wadau pia walisisitiza umuhimu wa kuhakikisha majiko yanawafikia wakazi wa maeneo ya mijini nchini Tanzania kwa bei nafuu, pamoja na kujadili njia za kuwafikia vikundi vya wanawake waliopangwa katika maeneo ya mijini na jinsi wanavyoweza kulipa kwa awamu ndogo kila mwezi.

Maswali na maoni yote haya yalijibiwa kikamilifu na kwa kuridhisha na waandaaji wa mradi.

**Uwasilishaji wa Kanuni za Ulinzi na Tathmini ya Uendelevu wa Mradi:**

ECCS1 na washirika wao walioteuliwa walielezea Kanuni za Ulinzi wa Mradi na tathmini yake. Wadau waliendelea kushauriwa na kushirikishwa kwa maoni na mrejesho kupitia majadiliano ya wazi. Mkutano uliendelea kwa wasilisho kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na athari chanya za mradi kwa baadhi ya Malengo hayo maalum. Washiriki walikubaliana na tathmini iliyowasilishwa na hawakuwa na maoni zaidi. ECCS1 pamoja na washirika wake walioteuliwa pia waliwasilisha mfumo wa kushughulikia malalamiko pamoja na njia ya kufuatilia athari za maendeleo endelevu.

**Hitimisho la Mkutano:**

Fomu za tathmini zilisambazwa kwa washiriki.

Timu ilitoa shukrani zake kwa washiriki wote walioudhuria mkutano huo na ambao walitoa mapendekezo mengi ya kujenga.

Mkutano ulifungwa kwa maonesho ya matumizi ya majiko ya Ecoa

**MAONI YALIYOPATIKANA KUTOKA KWA WADAU**

| Jinsia ya Mshiriki | Maoni ya Wadau | Maoni yalizingatiwa (Ndio / Hapana)? | Maelezo (Kwa nini? Vipi?) |
|---|---|---|---|
| M | Nikinunua jiko la umeme la Ecoa Induction, ni nini kinajumuishwa katika kifurushi? | Ndio | Jiko la umeme la Ecoa Induction linakuja na vyungu viwili vya kupikia na sahani moja ya kukaangia, na wanufaika watalipa kwa mfumo wa PayGo (malipo kwa awamu). |
| F | Je, ECOA hutengeneza majiko ya umeme pekee? | Ndio | Ecoa Climate Capital hutengeneza bidhaa za nishati ya mimea (Biomass) na za umeme, lakini kwa mradi huu, Effective Climate Solutions itasambaza bidhaa yetu ya umeme, jiko la Ecoa Induction. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| F | Jiko linaonekana dogo na linafaa zaidi kwa matumizi ya nyumbani.Vipi kuhusu taasisi na mashirika yanayohitaji majiko makubwa zaidi kwa mahitaji yao ya kupikia? | Ndio | Jiko la Ecoa Induction linafaa kwa matumizi ya nyumbani na biashara ndogo ndogo pekee. Hata hivyo, tutawaarifu wananchi mara tu majiko ya induction kwa matumizi ya taasisi yatakapopatikana katika siku zijazo. |
| F | Jiko linaonekana kuwa na uso wa kioo na linaonekana kuteleza. Nawezaje kuwa na uhakika kwamba wakati wa kupika vyakula kama ugali, sufuria haitateleza au jiko halitavunjika? | Ndio | Jiko la Ecoa Induction linakuja na zulia maalum la kupikia la siliconi linalosaidia kushikilia sufuria imara na kuzuia kuteleza wakati wa kupika. Kioo cha jiko ni imara sana na hakivunjiki kwa urahisi iwapo litatumika kwa uangalifu. |
| M | Ikiwa nitanunua jiko kwa mkopo na nimalize kulipa mkopo kabla ya miaka miwili, je, huduma za matengenezo zitapatikana endapo jiko litaharibika? | Ndio | Ndio, Ecoa Climate Capital itatoa huduma za matengenezo kwa bidhaa hata baada ya muda wa dhamana kuisha. Bidhaa zilizo ndani ya kipindi cha dhamana zitakarabatiwa bila malipo, na kwa bidhaa nje ya dhamana, matengenezo yatatolewa kwa gharama nafuu. |
| F | Dhamana ya jiko lenu la umeme inashughulikia aina gani ya uharibifu? Kwa mfano, ikiwa nitaliangusha kwa bahati mbaya na likaacha kufanya kazi, je, linaweza kubadilishwa? | Ndio | Ndio, Ecoa Climate Capital itatoa huduma za matengenezo kwa bidhaa hata baada ya muda wa dhamana kuisha. Bidhaa zilizo ndani ya kipindi cha dhamana zitakarabatiwa bila malipo, na kwa bidhaa nje ya dhamana, matengenezo yatatolewa kwa gharama nafuu.<br>Hata hivyo, dhamana haihusishi uharibifu unaotokana na matumizi mabaya au kushughulikiwa visivyo. Kwa uharibifu unaotokana na matumizi mabaya, mtumiaji atalipia gharama za matengenezo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| F | Ikiwa mteja anataka kununua jiko jingine, je, nambari ya mfululizo itabaki ile ile au watapewa jiko jipya lenye nambari mpya ya mfululizo? | NDIO | Kila jiko linakuja na nambari ya mfululizo ya kipekee. Hata hivyo, kwa majiko yanayohusiana na mradi wa kaboni, tunasambaza jiko moja kwa kila kaya pekee. |
| M | Vipi kuhusu watu wanaoishi maeneo ya vijijini ambapo umeme wa TANESCO haujafika, lakini jamii bado inahitaji majiko ya Ecoa? | NDIO | Kwa wateja wanaoishi maeneo ya vijijini ambao hawajajungwa na gridi ya umeme, tuna majiko mengine ya kupikia safi kutoka Ecoa Climate Capital, kama vile majiko ya Ecoa Wood na Ecoa Char. |
| F | Kwanini mteja anafuatiliwa baada ya kununua jiko ili kuhakikisha kama wanakitumia kwa kupikia au la, wakati inapaswa kuwa ni uamuzi wao binafsi kama watakitumia au la? | NDIO | Effective Climate Solutions na washirika wake watatoa elimu kwa wanufaika wakati wa usambazaji, na kwa mradi huu tutauza majiko tu kwa kaya zinazokubali kutembelewa kwa ajili ya zoezi la ufuatiliaji kama sehemu ya mahitaji ya kaboni. Mteja atapitia mchakato wa kuachia haki za mikopo ya kaboni. Hata hivyo, watu ambao hawataki kutembelewa wanaweza kununua bidhaa kupitia njia zetu za B2B (biashara kwa biashara). |

## MUHTASARI WA TATHMINI YA KANUNI ZA ULINZI

Wakati wa mkutano, ilielezwa kuwa lengo la mradi huu ni kusambaza majiko safi yenye ufanisi mkubwa ambayo yatapunguza matumizi ya mkaa na kuni katika kaya. Kwa njia hii, mradi utakuwa na athari chanya za kijamii, kiuchumi, na kimazingira. Mradi utafuata kanuni zote za ulinzi kama ilivyoelezwa kwenye jedwali hapa chini.

| **Kanuni za Ulinzi** | **Tathmini** |
|---|---|
| Haki za Binadamu | Mradi unaheshimu haki za binadamu zinazoainishwa kimataifa na hauhusiki katika vitendo vya unyanyasaji au ukiukaji wa haki za binadamu kwa namna yoyote ile, kama inavyobainishwa kwenye Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu. Mradi hautabagua washiriki katika kushiriki na kujumuishwa. |
| Usawa wa Kijinsia na Haki za Wanawake | Shughuli za mradi hazihamasishi aina yoyote ya ubaguzi wa kijinsia. Mradi utazingatia majukumu ya kijinsia na uwezo wa wanawake na wanaume |

| | |
|---|---|
| | kushiriki katika maamuzi na usanifu wa shughuli za mradi. Wanawake, pamoja na vyama vya wanawake, na wanaume wataalikwa kushiriki katika mashauriano ya wadau ili kuhakikisha uwakilishi wa kijinsia katika mikutano ya mashauriano |
| Afya ya Jamii, Usalama na Hali za Kazi | Mradi hautaweka jamii katika hatari kubwa ya kiafya na hautaathiri vibaya afya ya wafanyakazi na jamii. |
| Urithi wa Kitamaduni, Jamii za Asili, Uhamishaji na Uhamishwaji | Shughuli za mradi hazitakuwa na athari mbaya kwa urithi wa kitamaduni, jamii za asili, wala hazitasababisha uhamishaji au uhamishwaji wa watu. |
| Ufisadi | Mradi hautahusisha, kushiriki, au kwa namna yoyote kuchangia au kuimarisha ufisadi au miradi ya kifisadi. |
| Athari za Kiuchumi | Mradi utaheshimu haki zote za wafanyakazi. Hakuna athari mbaya za kiuchumi zinazotarajiwa kutokana na shughuli za mradi. Kinyume chake, mradi unatarajiwa kuchangia ukuaji wa uchumi endelevu |
| Hali ya Hewa na Nishati | Mradi utapunguza uzalishaji wa gesi chafu (GHG) kama itakavyofuatiliwa na kuthibitishwa kwa mujibu wa viwango vya kaboni |
| Maji | Mradi hautaathiri mtiririko wa maji ya asili wala kusababisha mmomonyoko wa udongo au kuyumbisha miili ya maji. |
| Mazingira, Ikolojia na Matumizi ya Ardhi | Mradi hautakuwa na athari mbaya kwa mazingira na ikolojia, na hautatumia ardhi na udongo kwa ajili ya uzalishaji wa mazao au bidhaa zingine. Utoaji wa chembechembe na monoksidi ya kaboni utapunguzwa kwa kiasi kikubwa kwa kuanzishwa kwa majiko bora zaidi |

| | |
|---|---|
| | yenye ufanisi mkubwa. |

Mchakato wa tathmini ulikuwa wa ushirikiano na ushiriki wa wadau. Wadau walikubaliana kikamilifu na tathmini iliyofanywa na ECCS1 na washirika wao.

## MUHTASARI WA TATHMINI YA UENDELEVU

Mradi huu utachangia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kwa njia zifuatazo:

| SDGs | Malengo | Kiashiria cha Ufuatiliaji |
|---|---|---|
|   | Kufikia mwaka 2030, kuhakikisha kuwa wanaume na wanawake wote, wakiwemo maskini na wale walio katika mazingira magumu, wanapata haki sawa za rasilimali za kiuchumi, pamoja na huduma za msingi, umiliki na udhibiti wa ardhi na mali zingine, urithi, rasilimali za asili, teknolojia mpya inayofaa, na huduma za kifedha, ikiwemo mikopo midogo. | Akiba ya fedha inayohusiana na ununuzi wa mkaa.<br>Utafiti utafanywa ili kuchunguza kiasi cha pesa kinachotumika kununua mkaa katika hali ya mradi ikilinganishwa na hali ya awali. |
|   | 3.9 Kufikia mwaka 2030, kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya vifo na magonjwa yanayosababishwa na kemikali hatarishi na uchafuzi wa hewa, maji, na udongo | Ubora wa hewa unaotambuliwa<br>Utafiti utafanywa ili kuchunguza athari za uchafuzi wa mazingira (kama vile viwango vya moshi, kuwashwa kwa macho, na matatizo ya kupumua) katika hali ya mradi ikilinganishwa na hali ya awali.. |

| **SDGs** | **Malengo** | **Kiashiria cha Ufuatiliaji** |
|---|---|---|
| 4 QUALITY EDUCATION | 4.3 Kufikia mwaka 2030, kuhakikisha kuwa wasichana na wavulana wote wanakamilisha elimu ya msingi na sekondari ya bure, yenye usawa na ubora inayosababisha matokeo ya kujifunza yanayofaa na yenye ufanisi.. | Idadi ya watu wanaopokea mafunzo ya ujuzi |
| 5 GENDER EQUALITY | 5.4 Kuhakikisha ushiriki kamili na wenye ufanisi wa wanawake pamoja na fursa sawa za uongozi katika ngazi zote za maamuzi ya kisiasa, kiuchumi na maisha ya umma.. | Ufanisi wa majiko bora husaidia kupunguza muda wa kupika na pia kupunguza mara za kununua mafuta ya kupikia. Hii huokoa muda, hasa kwa wanawake na wasichana, ambao mara nyingi hufanya kazi zisizotambuliwa za kukusanya kuni na kupika, na hivyo kuwawezesha kushiriki katika shughuli nyingine za maendeleo, mafunzo au ushiriki wa kijamii. |
| 7 AFFORDABLE AND CLEAN ENERGY | 7.1 Kufikia mwaka 2030, kuhakikisha upatikanaji wa huduma za nishati za kisasa, nafuu na za kuaminika kwa wote.<br>7.B Kufikia mwaka 2030, kupanua miundombinu na kuboresha teknolojia kwa ajili ya kusambaza huduma za nishati endelevu katika nchi zinazoendelea, nchi zilizo na maendeleo duni, nchi ndogo za visiwa vinavyoendelea, na nchi zisizo na pwani, kwa mujibu wa mipango yao ya usaidizi. | Idadi ya majiko bora ya kupikia (ICS) yaliyouzwa/kusambazwa na yanayotumika<br>Jumla ya ICS zilizouzwa/kusambazwa inahesabiwa kwenye hifadhidata. |

| SDGs | Malengo | Kiashiria cha Ufuatiliaji |
|---|---|---|
| 8 DECENT WORK AND ECONOMIC GROWTH | 8.5 Kufikia mwaka 2030, kuhakikisha ajira kamili na yenye tija na kazi nzuri kwa wanaume na wanawake wote, wakiwemo vijana na watu wenye ulemavu, pamoja na mshahara wa usawa kwa kazi ya thamani sawa. | Idadi ya ajira zilizoundwa |
| 13 CLIMATE ACTION | 13.3 Kuboresha elimu, uhamasishaji, na uwezo wa binadamu na taasisi katika kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, kukabiliana nayo, kupunguza madhara na kutoa tahadhari za mapema. | Kiasi cha kupunguzwa kwa uzalishaji wa $CO_2$ kutokana na shughuli za mradi |
| 15 LIFE ON LAND | 15.3 Kufikia mwaka 2020, kukuza utekelezaji wa usimamizi endelevu wa aina zote za misitu, kusitisha ukataji miti, kurejesha misitu iliyoharibiwa, na kuongeza kwa kiasi kikubwa upandaji wa miti duniani kote.. | Kupungua kwa matumizi ya kuni na mkaa.<br><br>Utafiti na ufuatiliaji wa mwenendo wa matumizi ya kuni katika kaya za mradi ikilinganishwa na kaya za awali ili kutathmini athari kwa rasilimali za misitu |

Tathmini ya maendeleo endelevu ya wadau ilikuwa sambamba kabisa na tathmini ya ECCS1 na washirika wao. Kuhusu ufuatiliaji wa viashiria vya maendeleo endelevu, wadau hawakuwa na maoni au mapendekezo mengine. Walikubaliana kuendelea na viashiria vilivyochaguliwa na ECCS1 na washirika wao.

**WASILIANA NASI:**
Ikiwa ungependa kupata maelezo zaidi kuhusu mradi huu, tafadhali wasiliana nasi kupitia:

| | **Njia Iliyoteuliwa (jumlisha maelezo yote yanayojulikana, kama eneo la kitabu, namba ya simu, utambulisho wa msuluhishi)** | **Sababu ya Kuchagua Njia Hii (utaratibu bora wa utekelezaji)** |
|---|---|---|
| **Mchakato Endelevu wa Maoni / Kitabu cha Malalamiko (lazima)** | BURN Manufacturing Tanzania Office.<br>Warehouse No.1<br>Plot No.544/1 Kawe Beach<br>P.o box 35792<br>Mwai Kibaki road<br>Dar es Salaam | Wadau walifurahia kuwepo kwa kitabu cha maoni katika ofisi kuu ya BURN. Malalamiko au wasiwasi wowote yanaweza kurekodiwa moja kwa moja katika ofisi kuu. |
| **Mawasiliano ya GS (lazima)** | help@goldstandard.org | Lazima kwa miradi ya Gold Standard |
| **Kupatikana kwa Simu (hiari)** | BURN: +255800750334 | Nambari ya simu ya ofisi ya BURN Kenya itajulikana kwa wanufaika wote wa mradi |
| **Kupatikana kwa Mtandao / Barua Pepe (hiari)** | customercare.tz@burnmfg.com | Anwani ya barua pepe ya BURN itajulikana kwa wanufaika wote wa mradi |